JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO WA KUSHIRIKI KATIKA SHINDANO LA UBUNIFU (INCLUSIVE & SECURE AI FOR EVERYONE HACKATHON 2026)

Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa kushirikiana na Taasisi ya CyberPeace pamoja na Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya Habari (WSIS) na waratibu wake, wanawaalika wadau wote kushiriki katika shindano la ubunifu la **Inclusive & Secure AI For Everyone (iSAFE) Hackathon 2026.**

Shindano hili la **iSAFE** ni shindano la ubunifu la kimataifa lililoundwa kupitia mkutano wa WSIS ili kuimarisha usalama wa mtandao, uaminifu wa kidijitali, pamoja na matumizi ya Akili Unde yenye maadili.

Shindano liko wazi kwa washiriki binafsi au kundi lisilozidi watu watatu kutoka duniani kote. Washiriki watasajili, kuwasilisha mawazo ya suluhisho, kisha kupita kwenda hatua ya mchujo, na ushauri wa kitaalamu (mentorship), na kufanya mawasilisho ya mwisho kwa njia ya mtandao.

Washiriki 20 bora watachaguliwa kuingia hatua ya mwisho, ambapo wataongozwa na wataalamu kutoka Umoja wa Mataifa, sekta binafsi, vyuo vikuu, na wataalam wa sera ili kuboresha mawazo yao. Maelezo zaidi yanapatikana kupitia kiunganishi hiki: https://www.itu.int/net4/wsis/forum/2026/en/Home/Hackathon

TCRA inawahamasisha wadau wote, wakiwemo wanafunzi, watafiti, wabunifu, watengenezaji wa mifumo ya kompyuta na wajasiriamali chipukizi kushiriki katika shindano hili la kimataifa ili kuchangia katika kuimarisha usalama wa mtandao, kuongeza uaminifu wa kidijitali, na kukuza matumizi sahihi ya teknolojia za kisasa.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Machi, 2026. Tafadhali jisajili kupitia kiunganishi hiki: https://www.cyberchallenge.net/registration

Imetolewa tarehe **19 Machi, 2026**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Thu Mar 19 17:43:30 EAT 2026

Dkt. Jabiri K. Bakari

**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz